
SMECAO FUND

S.L.P 87, SAME – KILIMANJARO

E-mail: smecao@gmail.com

Website: smecao.jimdo.com

MATUMIZI BORA YA JIKO LA KISASA LA KUNI – MUUNDO WA SMECAO

(SMECAO WOOD STOVE DESIGN)

Ufanisi bora wa jiko hili utawaliwa na vitu vifuatavyo:

1. Utawala wa moto/ kasi ya uwekaji kuni
2. Aina ya kuni zitumikazo
3. Umbali kati ya chombo cha kupikia na miale ya moto

UTAWALA WA MOTO/KASI YA UWEKAJI KUNI

Wingi/ ukali wa moto hutegemea ujazo wa hewa ya moto inayopanda kwenye bomba la moshi(chimney), ambayo huwa sawa na hewa iliyoingia kwenye mlango wa jiko hivyo kupuliza moto.

Ni lazima basi bomba la moshi liwe la kadri na liwe la bati kupunguza au/na kuongeza moto ili kutawala hewa moto inayopanda.

AINA YA KUNI ZINAZOTUMIKA

Kuni mbichi husababish akuziba kwa muda mfupi bomba la moshi kutokana na Utoaji nta ya moshi(charcoal tar) kwa kiwango kikubwa, hivyo basi yashauriwa kutumia kuni zilizokauka vizuri

UMBALI KATI YA CHOMBO CHA KUPIKIA NA MIALE YA MOTO

Ni vyema pawepo umbali wa centimeta 15 hadi 16 kutoka moto unapowaka hadi chombo cha kupikia.

Hivyo endapo Utoaji majivu wa mara kwa mara utaathirisha kuchimbika shimo kwenye jiko ni vyema lijazwe kwa vipande vya mawe na tope ili umbali uliotajwa hapo juu uwepo.

MENGINEYO

- UTUNZAJI WA JIKO:

1) Bomba

Huziba mara nyingi hivyo kusababisha uwakaji hafifu wa moto na moshi kurudi ndani. Ni lazima basi lisafishwe baada ya kipindi cha miezi sita ili kutoa mgandamano wa moshi ili kuwezesha hewa kupita.

La kufanya

Chukuwa jani refu bichi la mgomba na utoe sehemu yake pana ili ibakie ya katikati au fito iliyofungwa brashi ya katani iingize kwenye bomba la moshi kwa juu ili kuzibua moshi ulioganda. Pitisha mkono kwenye sehemu ya chungu cha pili ili kiganja cha mkono kifike kwenye mlango wa bomba kwa chini ili utoe unga wa moshi ulioganda.

2) Jiko zima

Japo limejengwa kwa mawe na udongo ni kawaida kuona mipasuko/nyufa kwenye jiko lenyewe ambazo zikiachwa zaweza kubomoa jiko lote

La kufanya

Tumia tope laini kuziba nyufa hizi mara zitokeapo, jiko likisiribwa kwa tope laini laweza kuwa na sura nzuri ya kuvutia.